MWONGOZO WA KUSAHIHISHA DIRA 10: FASIHI

1a) Jazanda / Sitiari

Maana; maelezo ya kimafumbo yanayoashiria jambo fulani au hali fulani inayofahamika kubeba hali nyingine tofauti.

i)Uvundo uliohanikiza katika eneo la soko la chapakazi unaoashiria uozo wa kijamii kama vile utepetevu wa viongozi.

ii)Uchongaji wa kinyago kizuri cha mwanamke ambaye ni Tunu akiwa na kinasa sauti ni kuanagazia nafsi ya mwanamke katika jamii: ana uwezo wa kuwa kiongozi.

iii)Uchongaji wa kinyago cha mhenga fulani wa Boza unaashiria uhafidhina na ubarakala unaoendelezwa katika jamii na baadhi ya watu.

iv)Kombe anaposema kwamba keki ya uhuru imeliwa kwingine kisha wao waletewa masazo kuonyesha utabaka na ukoloni mamboleo unaoendelezwa na viongozi na vibaraka wao wanaojifaidi pekee.

v)Majoka anapomwambia Ashua kuwa hangeacha kula mkate kwa kuchelea kiungulia. Hali hii inaashiria uendelezaji wa anasa na uozo wa viongozi wanaotaka kutumia madaraka ya kutimiza ufuska wao hata kwa wake wa watu bila hofu yoyote.

vi)Kenga anaposema kuwa ukitaka kuwafurusha ndege kata mti kwa maana ya kuangamiza viongozi wa makundi pinzani inadhihirisha maudhui ya ukatili na siasa za mauaji.

vii)Sudi anapomwambia Ashua kuwa siasa yao imesukumiza kwenye chombo wasichotaka kuabiri anamaanisha imebidi washiriki katika harakati za ukombozi. Aidha, maudhui ya asasi ya ndoa yanaangaziwa kupitia mzozo wao. (Sudi na Ashua)

vii)Chopi anawaambia Sudi kuwa shamba likimshida kulima aseme anaamanisha pengine Sudi ameshidwa kumkidhia Ashua mahitaji yake kama mke hivyo kuendeleza maudhui ya ndoa na mapenzi.

viii)Babu anasema kuwa chombo chenye rubani imara huhimili vishindo na hasira ya mawimbi kumaanisha uongozi mzuri hutegemea kiongozi aliyeimara na mwajibikaji.

ix)Babu anaporejelea mshumaa kuwaka na kuwasha mishumaa mingine anamaanisha kiongozi anastahili kuwafaa raia. Aidha, anadokezea umuhimu wa umoja na ushirikiano katika jamii.

x)Ashua anamwambia Majoka kuwa ushahidi hauwezi kupatikana ikiwa kipanga ndiye hakimu katika kesi ya kuku kumaanisha ukiukaji wa haki katika jamii.

xi)Babu anamwambia Majoka kuwa labda chombo chake kinakwenda kinyumenyume badala ya kwenda mbele kumaanisha utawala wa Majoka haujaonyesha mabadiliko yoyote yaliyoleta manufaa bali umeendeleza ukoloni mamboleo.

MAJAZI

b) i) Majoka -nyoka kubwa kupita kiasi. Ana tabia ya nyoka kubeba fimbo ya nyoka na maumbo ya nyoka. Kutengeneza sumu ya nyoka. Kufuga nyoka(swila)

ii) Tunu –kitu cha dhamana(zawadi)
ni mwanamke wa kipekee anayekabiliana na viongozi dhalimu.

iii) Sudi -bahati njema. Ni bahati njema kwa Sagamoyo. Anajitolea kupigana na uongozi mbaya.

iv) Kenga-kumfanya mtu aamini jambo lisilo la kweli (uongo)

v) Husda-kuonea mtu gere/ kijicho/wivu. Anamwonea Ashua wivu kwa sababu amesoma, mrembo na apendwa na Majoka.

vi) Kombe-mmea unaotambaa ambao utomvu wake ni sumu inayopakwa katika kigumba cha mshale.
Ana tabia ya kutoonyesha msimamo dhabiti.

vii) Ngurumo- sauti ya mvumo inayosikika angani wakati wa mvua. Anahusika kuwaua na kuwapiga wapinzani wa Majoka

viii) Chopi-kulewa chopi/ chakari. Hakufuata maagizo anayopewa na Majoka kwa sababu ya kulewa.

ix) Mama Pima-kazi yake ni kupima na kuuza pombe

x) Asiya-sehemu ya kitu au mbaki. Mfano Majoka anamuona kama mbaki linalostahili kuondolewa baada ya kifo cha Ngurumo.

xi) Boza-mjinga/ mpumbavu. Mfano anaunga mkono serikali kijinga, mkewe azini na Ngurumo.

xii) Hashina-mwenye heshima, anawafundisha wengine kuwa na heshima.

xiii) Saga moyo-kufanya kitu kiwe unga unga(saga) . Watu wanaoishi katika jimbo hili wanapitia maumivu makali ya moyo.

xiv) chapakazi- mahali pa kufanyia kazi kwa bidii.
Zozote 10 x 1 = 10

RIWAYA CHOZI LA HERI

2. (a) Sauna anakumbuka maneno aliyoambiwa na mamaye kumhusu Bwana Maya aliyekuwa baba yake wa kambo na aliyembaka. Anawaza haya akiwa kwa Bi Kangara anapokabiliwa na polisi wanaomtafuta kwa kosa la ulanguzi wa watoto.

(b) Umulkheri mwana wa Lunga

- Yeye na ndugu zake waliachwa na Wazazi wakiwa wadogo.
- Ndugu zake Dick na Mwaliko wanatoroshwa na kijakazi Sauna.
- Juhudi za kupata msaada wa polisi kuwatafuta zinagonga mwamba.
- Katika umri huo mdogo anaondoka kwao na anajikuta katika jiji.
- Inabidi aishi na Apondi na Mwangeka kama mtoto wa kupanga na kukosa mapenzi ya wazazi.

Apondi

- Ni mjane kwani mumewe alifia ughaibuni.
- Anawachiwa jukumu la kumlea Sophie, kitoto cha miaka miwili.
- Anaishi maisha ya upweke na huzuni.
- Aliogopa kupata mume mwingine kwa kuchelea kuachwa tena.

Mwanaheri, mwanawe Kaizari

- Alifukuzwa kutoka kwao miaka baada ya vita vya kikabila vya miaka mitano ya awali.
- Katika ghasi 'za vita yeye na dadake walibakwa mbele ya wazazi wao.
- Mama yao aliwaacha baada ya kukosana na mama mkwe.
- Baba yao alikufa baada ya kifo cha mama.

Kairu

- Hawana pa kwenda baada ya kufurushwa wakati wa vita.
- Wanapopata makao kwenye kambi wanaishi katika kibanda kidogo na wazazi.
- Kitindamimba wao anapoteza maisha.
- Biashara ya mamake si imara kutokana na migogoro kuhusu kisiwa wanakotoa samaki.
- Kwa kuwa alizaliwa nje ya ndoa, inakuwa vigumu kupata msaada kwa babake.

3.**Haki za binadamu hujumuisha mambo au vifaa ambavyo mtu anahitajika kupata au kupokea na kanuni za jamii yake. Katika Chozi la Heri kuna:**

a) Uharibifu wa mali. Kwa mfano, jumba la Ridhaa la kifahari linateketezwa bila huruma na waandamanaji wanatupia magari mabomu ya petroli.

b) Mauaji. Polisi wanakabiliana kikatili na uhalifu wa vijana, wanawapiga risasi. Familia ya Ridhaa inachomewa ndani ya nyumba, raia wanamchoma Lemi, watu wanaavya mimba na kuvitupa vijusi kwenye majaa (uk. 161).

c) Kupigwa. Subira, mkewe Kaizari, anapigwa na kukatwa na wanaharakati kwa madai kwamba Kaizari alimuunga mkono Mwekevu.

d) Unyanyasaji wa kimapenzi. Vijana wanawabaka Lime na Mwanaheri, Sauna anabakwa na Bwana Maya, baba yake wa kambo.

e) Dhiki ya kisaikolojia. Mabarobaro wanawabaka Mwanaheri na Lime mbele ya baba yao. Wanaondoka bila hata kumgusa Kaizari ambaye anabaki kuuguza donda la kihisia. Babake Zohali anamsimanga na kumwambia atasaidiwa ulezi na baba mtoto.

f) Kutengwa. Mavyaa wa Subira anamchukulia kama mgeni; anasema msichana wa Bamwezi hubakia msichana hata angawa na umri wa miaka tisini. Anamwona kama aliyesababisha kuhujumiwa kwa mali yao (uk. 94).

g) Kutelekeza malezi. Subira anawaacha watoto wake bila kujali huzuni anayowasababishia. Naomi anawaacha mumewe na watoto japo anajua hali

h) Ulanguzi wa watoto. Sauna akishirikiana na Bi. Kangara wanaendeleza wizi wa watoto. Wanawateka nyara na kuwapeleka wengine kwenye madanguro na wengine kufanya kazi ughaibuni, na kwenye mashamba na makasri ya matajiri (uk. 158), Sauna anawaiba Dick na Mwaliko.

i) Ajira ya watoto. Mzee Buda anawaajiri watoto. Anamtumia Dick kulangua dawa za kulevya ughaibuni. Pete anamtumia mtoto mdogo kumlindia mtoto wake (uk. 150).

j) Unyanyasaji wa kijinsia. Bwana Maya anampiga Mama Sauna na hali mama huyu anakubali chochote anachoambiwa (uk. 154).

k) Ukiukaji wa haki za wagonjwa. Dawa zinazonuiwa matumizi ya wagonjwa zinaishia kwenye maduka ya dawa ya msimamizi wa hospitali (uk. 140).

l) Ukiukaji wa haki za wafanyakazi. Selume analalamikia ukosefu wa vifaa vya kimsingi kama vile glavu (uk. 139) na huduma za umeme (uk. 140). Kimondo analalamikia ujira duni unaopewa wafanyakazi katika shamba la kahawa (uk. 69), wafanyakazi hawana bima ya matibabu kwani wanasemekana ni vibarua (uk. 70). Baba yake Shamsi anakufa kwa ukosefu wa dawa kwenye hospitali ya kijijini na kwenye hospitali ya wanyonge mjini (uk. 135).

m) Kunyimwa haki ya kujua/kupata habari. Mama yake Sauna hamwambii Sauna kuwa Bwana Maya si baba yake halisi. Mama yake Kairu hamwambii Kairu sababu ya kutomwomba Baba Kairu amlipie karo (uk. 93). Mama yake Pete anamtelekezea kwa nyanya yake bila hata kumwambia kiini cha kutofanana na baba yake. Anaambiwa na mtu mwingine kuwa mama alimpeleka kwa nyanya kwa kuhofia kusambaratisha ndoa yake.

n) Kunyimwa haki ya elimu. Pete anaozwa licha ya rai za nyanya yake kwamba aachwe afuatilie elimu (uk. 148).

o) Kunyimwa haki za unyumba. Mkewe Kiriri, Annette, anahamia ng'ambo na kumwacha mumewe kwa upweke. Anasema amemwachia vimada wake. Naomi anamwacha mume wake, Lunga.

p) Kutotetewa kwa vijana wa kiume ambao wanalawitiwa (uk. 17).

q) Kesi kukawia kwa muda mrefu bila kusikilizwa. Tila ana matumaini kuwa jaji ili kesi ambazo zinaselelea mahakamani kwa miongo miwili zisikilizwe na kuamuliwa (uk. 45).

r) Ukiukaji wa haki za wafungwa. Wanawekwa rumande kwa muda mrefu, miongo miwili huku wakingojea kusikilizwa kesi (uk. 45).

s) Taka kutoka maeneo ya walio nacho kuelekezwa kwenye mtaa wa Sombera ambapo wanyonge kama vile Makiwa wanaishi (uk. 28).

t) Wanyonge kwenye Msitu wa Mamba kupewa hatimiliki huku uongozi ukijua kwamba ardhi hii ni marufuku.

u) Uongozi unaruhusu ujenzi wa nyumba kwenye maeneo yaliyotengewa ujenzi wa barabara, na baadaye kuwasababishia wenyewe hasara kwa kuyabomoa. Ridhaa anabomolewa majumba yake matatu.

v) Kuachishwa kazi. Lunga anafutwa kazi kwa kupinga kuuzwa kwa mahindi duni kwa raia.

HADITHI FUPI

4. Mapenzi Kifaurongo

(a) "Hadi sasa mimi ni kama rubani aliyeharibikiwa na ndege angani." Onyesha ukwelii wa dondoo hili.

(swali linatahini matatizo aliyokumbana nayo Dennis)

- Dennis alitokea katika familia ya kimaskinina hanhemudu mavazi mazuri kama ya wenzake chuoni au vifaa meme vya kisasa kama vile ipad, tarakilishi n.k.
- Dennis hakusomea shule za kifahari kama wenzake chuoni.
- Somo la Daktari Mabonga linamvunja moyo Dennis na anahisi hapo hapamweki kwa vile namna anavyoendesha somo hilo anawatia fadhaa.(uk 14)
- Dennis anapomwomba mhadhiri atumie lugha nyepesi, darasa nzima linamcheka huku mwalimu akimkejeli kuwa iwapo alinuia kuwachekesha hajui kuchekesha.
- Dennis kinyume na wenzake hana pa kukimbilia mambo yanapoharibika chuoni- wengine wataajiriwa na jamaa zao huku wengine wakiwa na wachumba wanaofanya kazi za kifahari serikalini na watawafadhili na kuwaondoshea kero la elimu ya juu.
- Chuoni Dennis anaishi maisha duni. Malazi yake yamechanikachanika. Hana chakula na analazimika kupika uji mweupe na kuunywa kama chamcha.
- Dennis anatafuta kazi sana baada ya kufuzu kama mtangazaji wa redio- kazi kwake inakuwa ni kuitafuta kazi yenyewe.
- Dennis anakosa nafasi ya ajira kwenye shirika la kuchapisha magazeti. Kazi hiyo anapewa Shakila kwa sababuu mamake ni mkurugenzi wa kampuni hiyo- hapa anafanyiwa ubaguzi moja kwa moja.
- Baada ya Penina kutambua Dennis hakufanikiwa kupata kazi, hataki hata amwite mpenzi. Hampikii kwa sababu alipotoka asubuhi hakuchangia chochote.
- Penina anamfukuza Dennis pale kwao nyumbani na anamweleza asije akamwambia mtu kuwa waliwahi kuwa wepenzi.

  (Hoja 10x1=10)

(b) Shibe Inatumaliza

"Hatuwezi kumaliza kula. Kila leo tunakula. Hiki na kile…"

Fafanua dhana ya ulaji kama inavyojitokeza kwenye hadithi hii. (alama 10)

(swali linatahini ufisadi na ubadhirifu)

- Mzee Mambo hana kazi maalum, ni waziri kivuli wa wizara zote. Anakiri hana kazi hata moja. (uk 37)

- Nchi ya kina Mzee Mambo kinachoangaliwa ni kwenda kazini na si kufanya kazi.
- Mzee Mambo na wengine wenye vyeo hujipakulia mishahara waitakayo bali si kupokea mshahara.
- Sasa na Mbura wanaongoza wzara moja ya mipango na mipangilio. Wao hupanga na kupangilia hiki na kile kwa hiari yao au kwa kuamriwa na huyu na Yule. (uk. 38)
- Magari ya kiserikali kutumiwa vibaya kwenye sherehe ya Mzee Mambo.
- Kuwepo kwa watu fisadi serikalini wanaotajwakama wenye vyetu (uk 39). Hawa wanasemwa kuliteremsha jungu kutoka ikulu kwa gari la serikali.
- Wafanyabiashara kuagiza mchele kutoka ng'ambo ambao ni wa thamani ya chini na kupuuza ule unaozalishwa kwao (Mbeya)- wanapofanya hivi wanahasiri wakulima wa Mbeya.
- Kwenye sherehe kwa Mzee Mambo, DJ na wenzake wanachota mabilioni ya pesa kwa kuwachezea watu muziki.
- DJ anamiliki duka kubwa la dawa ambalo mtaji wake unatajwa ni bohari kuu la dawa za serikali (uk. 43)
- DJ na wenzake kupata huduma za kimsingi bure huku raia maskini wakilazimika kulipia huduma hizo.
- Sasa na Mbura kula vyao na vya wenzao- hata vya wale walioaga dunia tayari. (Hoja 10x1=10)

5. <u>Ndoto ya Mashaka</u>

Mwandishi wa hadithi hii anatupa taswira ya jamii iliyozongwa na masaibu yanayotamausha. Tetea ukweli wa kauli hii. (alama 20)

- Mashaka hakupata malezi mema- alikosa lishe bora. Chakula kilikuwa ni tikitimaji na matango.
- Mashaka katika umri mdogo aliwapoteza wazazi na kulelewa na Bi. Kidege.
- Mamake mlezi (Bi. Kidege) anakabiliwa na maradhi ya miguu hivyo anashindwa kuzumbua riziki yao.
- Mashaka anashiriki katika ajira katika umri mdogo ili wapate riziki yeye na mamake mlezi (uk. 72)
- Punde Mashaka anapokamilisha masomo ya chumba cha nane, mamake mlezi anaaga dunia na kumwacha katika ukiwa.
- Ndoa ya Mashaka haikuwa ndoa ya kutajika – ilikuwa ni ndoa ya kulazimishiwa licha ya umaskini wake.
- Mashaka anabaguliwa na Mzee Lubeya na mkewe ambao ni wakwe zake kwa umaskini wake. Wanalazimika kukimbilia Yemeni kukimbia aibu.
- Mashaka na mkewe Waridi kuishi kimaskini katika chumba kibovu. Anaeleza kuwa shida ziliwatamiria kila upande. (uk. 74)

- Mashaka na Waridi kuwazaa watoto wengi ambao wanashindwa kuwapa malezi mema. Watoto wa kike kulala chini kwenye chumba kimoja na mamao ilhali wale wa kiume waliombewa jikoni kwa Chakupewa walikolala kama nyau.(uk.75)
- Mazingira ya pale kwa kina Mashaka ni mabovu. Harufu ya choo kinachokumbatia chumba chao kuhamia chumbani mwao.Kuna mfereji wa maji chafu unaotema maji yake kwenye Mto Msimbazi (uk. 74)
- Mashaka na familia yake hawana choo- wanakwenda haja zote kwenye karatasi za plastiki na kuzitupa ovyo.
- Viongozi kusaliti raia wanyonge- waakati wa mafuriko huwatangazia wahame mabondeni lakini hawawapi makao bora. (uk. 75) – hawasemi waende wapi.
- Mshahara wa mkia wa mbuzi aliopewa Mashaka kazini haungemruhusu kununua vifaa vya nyumbani. Aidha nafasi ya chumba chao haingetosha.
- Waridi na watoto wanamtoroka Mashaka bila kuaga. Aliwahi kudokeza kuhusu kutoroka kwake katika wimbo ambao Mashaka hakuuelewa wakati huo. (uk. 77)
- Utengano na familia yake ulimpa Mashaka unyonge. Hakuona thamani ya maisha tena.
- Jamii ya kimataifa ilifumbia macho unyonge wa watu walioishi maeneo dunikama vile Tandale.
  (Hoja zozote 10x2=20)

6. USHAIRI

(a) Shairi huru

(b) (i)Lina beti

(ii) Lina mishororo

(iii) Kila ubeti unabeba ujumbe lake

(iv) Lugha ni ya kishairi

(c)

(i) Hisia zake zinamkumbusha mambo ambayo aliyasahau
(ii) Mambo yasiyovutia
(iii) Majonzi ya kitambo
(iv) Hapatani na hisia zake
(v) Anaomba hisia zake zitulie

(d)

(i) Tashihisi /uhuishi/uhaishaji
(ii) Nidaa
(iii) Mdokezo
(iv) Tashbihi

(e)

(i) Niloisahau-Niliyoisahau
(ii) Umesubutu- umethubutu

(iii) Mtimani- moyoni

7. USHAIRI

a) Dhamira

Mshairi analalamika / ananung'unika kuhusu kunyimwa haki na ameamua ataidai kwa vyovyote vile.

(1 x 2 = 2)

b) (i) Inkisari – Ili kutosheleza idadi ya mizani.

mf. 'taidai - nitaidai
alo - aliye

(ii) Kubananga sarufi – Kutosheleza vina.
mf. Haki yangu 'taidai – Nitaidai haki yangu.

(iii) Kikae / kikale – kutosheleza vina
mf. Maizi – jua / fahamu / elewa/ tambua
(iv) Udondoshaji – itaidai.

(mbili za mwanzo) 2 x 2 = 4

c) Hata uifungie haki yangu ngomeni na kuizingira kwa ua, usimamishe kitu cha thamani mbele yangu, bado nitasimama na kushikilia haki yangu kwani naelewa kuwa sifa kubwa kwangu kama mwanamme ni kwenda hata kama ni kwa kujikokota lakini haki yangu nitaidai kwa vyovyote vile. (5 x 1 = 5)

d) (i) Urudiaji wa maneno – haki, haki
(ii) Urudiaji wa silabi – <u>kina</u> ta, ta, ta
(iii) urudiaji wa vishazi - haki ifukue chini
- haki ijengee ngome

(zote 3 x 1 = 3)

e) (i) Takhmisa – mishororo mitano katika kila ubeti.
(ii)Ukara – vina vya nje vina urari (t<u>a</u>) na vya ndani vinabadilikabadilika.

(2 x 1 = 2)

f) Toni ya - uchungu
- hasira (yoyote 1 x 1= 1)

g) Nafsi neni - Mnyonge
- Anayedai haki yake
- Mwanamume anayedai haki

(yoyote 1 x 1 = 1)

h) (i) Kwa kila ala maizi hawi mithili ya bata -
Yule mwenye kutambua hawezi kulinganishwa na bata asiyejua lolote.

(kutaja 1, kueleza 1 - Jumla 2)

8. FASIHI SIMULIZI

(a) (i) Vitendawili

Mfano:- Nimemfukuza na sikumkuta (kivuli)

- Mungu kanipa viatu visivyokwisha (Nyayo za mguu)

(ii) Methali

Mfano:- Kuishi ni dhamiri

- Mwenda mguu hatambi

(iii) Misemo

Mfano: -Kukefyakefya – kusumbua si koleo wala si mani – mtu ovyo

(iv) Misimu

Mfano:- Sonko – tajiri

- Princi – mwalimu mkuu.
- Finje – shilingi hamsini

(v) Nahau

Mfano:- Mfua uji – mtu mtanashati

Mtoto wa kikopo –Mhuni

(vi) Vitanza ndimi

Mfano: - Sane ikipita sana huwa makosa sana.

- Sita, (jina la mtu) sitasita kusisitiza kuwa sita sio tisa.

(vii) Ishara

Mfano : - Kuwa na moyo wa kutu. (roho mbaya)

- Umekuwa lumbwi (kigeugeu)

Ataje nne (kutaja alama 1, mfano alama 1)

4 x 2 = 8

(b) Tamathali

(i) Tashbihi – sababu –ametumia kilinganishi kama. Alama 2

(ii) Sitiari /istiari – sababu –amelinganisha moja kwa moja. Alama 2

(iii) Kefeli – sababu – haweze kuwa shujaa kwa kuchukua fimbo. Alama 2

(iv) Tashhisi - sababa- kiburi kimepewa uhai. Alama 2

(jumla alama 8)

(c) (i) Mwasherati

(ii) Mwasherati

(iii) Mchoyo

(iv) Mtu maridadi